KANUNI YA MAADILI YA UWAJIBIKAJI YA WANAFUNZI

SCORE KWA MUHTASARI

2023-24

Mambo muhimu ili kuelewa sera za nidhamu za Shule za Umma za Richmond.

Lengo la SCORE ni kuendelea kuweka kigezo cha juu kwa wanafunzi wetu huku tukifahamu kwamba kwa kufanya hivyo lazima tutumie njia ambazo zinazingatia kiwewe na za kurejesha maadili. Hii inamaanisha kwamba ijapokuwa tunamaanisha kwamba wafanyakazi wa shule wanapaswa kushughulikia ipasavyo tabia ambazo zinaathiri vibaya mazingira ya shule, tunaamini pia kwamba tunaweza kuwasaidia wanafunzi kujifunza kutoka kwa makosa yao na kuwasaidia kufanya maamuzi bora baadaye. RPS itakuwa kitengo cha shule chenye lengo la kimakusudi la kujenga na kudumisha mahusiano na ambalo linapunguza matokeo makali ya kiadhabu kwa kuzingatia chaguo zinazowaweka wanafunzi shuleni, wakiwa wameshikamana na jumuiya ya shule zao.

Ni Lini na Wapi SCORE Inatumika

Viwango katika SCORE vinatumika kwa tabia:

- Kwenye mali ya shule, ambayo inajumuisha mali yoyote ya RPS inayomilikiwa au iliyokodishwa, inayoendeshwa na au kwa niaba ya Bodi ya Shule.
- Kwenye basi la shule, kwenye vituo vilivyoteuliwa vya basi, au kwenye njia za moja kwa moja za kwenda na kurudi kutoka shuleni.
- Wakati wa kushiriki, au kuhudhuria, shughuli zinazofadhiliwa/zinazohusiana na shule, kama vile safari za kielimu, makongamano au matukio za riadha.

Viwango vya Uingiliaji Kati na Ushughulikaji

SCORE inawawajibisha wanafunzi kwa tabia zao. Tabia zimepangwa katika viwango vitano kulingana na ukali wa tabia. Wakati wowote inapowezekana na inafaa, uingiliaji kati unapaswa kuanza kwa kiwango cha chini zaidi cha uingiliaji kati/ushughulikiaji. Walimu wakuu, walimu, wafanyakazi wa shule, wanafunzi na wazazi wanahitaji kufahamu mbinu za uingiliaji kati na/au ushughulikiaji zinazoweza kutumika wakati mwanafunzi anapokosea au kuvuruga darasa kwa kiasi kikubwa. SCORE imegawanywa katika sehemu mbili Chekechea hadi Gredi ya 5 na Gredi za 6 hadi 12 ili kuhakikisha kwamba umri na ukomavu wa jumla wa wanafunzi unazingatiwa.

Kiwango cha 1 Ushughulikiaji wa kiwango cha 1 unalenga kuzuia matatizo zaidi ya kitabia huku mwanafunzi akiendelea kuwa shuleni.

Kiwango cha 2 Uingiliaji kati na ushughulikiaji wa kiusimamizi wa kiwango cha 2 umebuniwa kama hatua za uzuiaji ili mwanafunzi aendelee kuwa shuleni na itategemea ukali wa tabia.

Kiwango cha 3 Tabia za kiwango cha 3 zinaweza kusababisha mwanafunzi kuondolewa shuleni kwa muda mfupi kulingana na ukali, asili sugu na maswala ya usalama.

Kiwango cha 4 Tabia za kiwango cha 4 zinaweza kuhitaji kuripoti tabia hio kwa mteule wa msimamizi na huluki nyingine. Rufaa kwa mteule wa msimamizi inaweza kusababisha kusimamishwa kwa muda mrefu, mabadiliko ya mpango au kufukuzwa kabisa. Baada ya ukaguzi, mteule wa msimamizi anaweza kuwarejesha wanafunzi kwenye mazingira yenye huduma za kina zilizo na usaidizi wa ziada.

Kiwango cha 5 Ushughulikiaji wa kiwango cha 5 umetengwa kwa ajili ya tabia zile zinazohitaji rufaa kwa mteule wa msimamizi. Kwa wanafunzi walio katika shule ya mapema hadi gredi ya tatu, kusimamishwa kwenda shule kwa zaidi ya siku tatu lazima kuwe na rufaa ya mteule wa msimamizi. Rufaa inaweza kusababisha kufukuzwa, mabadiliko ya mpango, kuhamishwa hadi shule nyingine, au kusimamishwa kwa muda mrefu.

Ushughulikiaji wa Kiwango cha 1	Ushughulikiaji wa Kiwango cha 2
Mlezi hupokea simu, barua au ombi la kuhudhuria mkutano.	Uwezekano wa mwanafunzi kuondolewa kwa muda mfupi kutoka darasani.
Hutambua na kutuza Tabia ifaayo.	Rufaa kwa Timu ya Uingiliaji Kati wa Tabia ya Wanafunzi (SBIT).
Hufundisha na kutoa mfano wa tabia inayotakikana.	Usaidizi wa ndani ya shuleni kwa uingiliaji kati wa tabia.
Mfumo wa Ukaguzi wakati wa Kuingia na Ukaguzi wakati wa Kuondoka.	Makubaliano ya tabia.
Utatuzi wa migogoro au makundi ya kukuza jumuiya.	Upatanishi wa rika.
Mkutano wa mwalimu na mwanafunzi.	Rufaa kwa mtaalamu wa tabia.
	Siku ya shule iliyoongezwa.

Maelezo kamili ya tabia, uingiliaji kati na ushughulikiaji yanapatikana katika ukurasa wa SCORE wa 10 hadi 17.

Taratibu za Kukata Rufaa Uamuzi wa Kusimamishwa Shule

SIKU 10 AU CHINI



Sera ya Mahudhurio ya Wanafunzi

Kuhudhuria ni muhimu kwa mafanikio ya kila mwanafunzi — kila siku ni muhimu! Wanafunzi hawapaswi kukosa shule (iwe kwa sababu zenye udhuru au zisizo na udhuru, bila kujumuisha siku za kusimamishwa) kwa siku **18 au zaidi** za shule kwa mwaka, au; vipindi **18 vya darasa** ya kozi fulani au siku **9 za shule** kwa kozi ya muhula mmoja.

Walezi lazima watume barua inayotoa tarehe na maelezo ya kutokuwepo shuleni, mnamo siku ambayo mwanafunzi anarudi shuleni. Iwapo barua haitatumwa **ndani ya siku 5 za shule** kutoka siku ya mwisho ya kukosa shule, kipindi hiki cha kutohudhuria kitachukuliwa kuwa hakina udhuru. Sababu za kutokuwepo kwa udhuru ni pamoja na:

- Ugonjwa binafsi, na ukichukua zaidi ya siku 3 shule itahitaji barua kutoka kwa daktari.
- Kuhudhuria mahakama binafsi.
- Msiba katika familia.
- Sikukuu za kidini zinazoadhimishwa mara kwa mara na mwanafunzi.
- Mambo makali, kama ilivyoidhinishwa na usimamizi wa shule.

Tazama kurasa za 35 hadi 37 katika SCORE kwa maelezo zaidi kuhusu Sera ya Mahudhurio.

KAZI YA KUFIDIA MUDA ULIOKOSEKANA

Kuomba Kazi ya Kufidia Muda Uliokosekana: Itakuwa jukumu la mwanafunzi na mlezi kuomba kazi ambazo hazikufanywa. Notisi ya saa 48 inahitajika ili kutoa kazi ya kufidia kwa mwanafunzi. Ikiwa kazi haipatikani kwa njia ya kielektroniki, inaweza kuchukuliwa katika ofisi kuu.

Kukamilisha kazi ya kufidia muda uliokosekana: Wanafunzi watapewa angalau siku nyingi za kufanya kazi ya kufidia kulingana na jumla ya siku ambazo hawakuhudhuria.

Vitabu vya SCORE vinaweza kupatikana katika shule zote. Tafadhali wasiliana na shule ya mtoto wako ikiwa una maswali yoyote.

Changanua Hapa

Ili kuona toleo kamili la SCORE au tembelea rvaschools.net/score.